بسم الله الرحمن الرحيم

# FADHILA ZA MWEZI WA SHAABAN NA UZUSHI WA NISFU SHAABAN

Imeandaliwa na: Yunus Kanuni Ngenda
Imepitiwa na: Abubakari Shabani Rukonkwa

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, na rehma na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad (s.a.w) na watu wake na Maswahaba wake wote. Amma baad:

Mwezi wa Shaaban ni mwezi wa nane katika kalenda ya Kiislam. Na ni mwezi ambao upo katikati ya miezi miwili mitukufu; Rajab na Ramadhaan. Mambo ya kuzingatia katika mwezi huu ni kuweza kupambanua yaliyo sahihi na yaliyozushwa, kwani ingawa kuna fadhila zake mwezi huu lakini pia mengi yaliyoenea na yanayofanywa na watu, ni ya Upotofu.

Ni mwezi ambao Mtume (S.a.w) alikuwa akifunga sana Swawm za Sunnah kama ilivyothibiti katika Hadiyth ifuatayo kutoka kwa Mama wa Waumini

‘Aaishah (R.a) “Mtume (S.a.w) alikuwa akifunga hadi tukadhani kuwa hatofungua kamwe, na alikuwa akiacha kufunga hadi tukadhani hatofunga tena. Sijamuona Mtume (S.a.w) akifunga mwezi mzima kama alivyokuwa akifunga Ramadhaan, na sijamuona akifunga mara nyingi kama alivyofunga katika Sha’abaan”

[Al-Bukhaariy na Muslim].

## SWAUMU NA FADHILA ZA MWEZI WA SHAABAN:

Juu ya kwamba Mtume (S.a.w) alikuwa akifunga mara nyingi zaidi katika mwezi wa Sha’abaan kuliko miezi mingine ukiondosha Ramadhaan, kama ambao unafungwa wote, hakuwahi hata mara moja kuufunga mwezi mzima wa Sha’abaan. Na ni jambo ambalo lenye kuchukiza kufanya hivyo kama wanavyotueleza wanachuoni kama kina Ibnul Mubaarak na wengi wengine, pia Swahaba mtukufu Ibn ‘Abbaas anasema ni makruhu kufunga mwezi mzima wa Sha’abaan kwani Mtume wa Allah hakufanya hivyo.

Imepokewa kuwa Ibn ‘Abbaas (R.a) amesema: ‘‘Mtume wa Allaah (S.a.w) hakuwahi kufunga mwezi wowote kikamilifu isipokuwa Ramadhaan.

[Al-Bukhaariy].

Kukithirisha kwake Mtume (S.a.w) ibada katika mwezi huu wa Sha'abaan, ni kutokana na maelezo yake mwenyewe alipoulizwa na Usaamah bin Zayd

(R.a) sababu ya kufunga sana katika mwezi huu alijibu: “[Sha'abaan] ni mwezi ambao watu hawautilii sana maanani, ulio kati (ya miezi miwili mitakatifu) Rajab na Ramadhaan, na ni mwezi ambao matendo yanapandishwa kwa Mola wa ulimwengu. Nami napenda matendo yangu yapandishwe na hali nikiwa nimefunga” [An Nasaaiy, at-Targhiyb wat-Tarhiyb, uk. 425].

Kufunga katika mwezi wa Shaaban ni mazoezi kabla ya Ramadhaan. Hata hivyo, kufunga mwezi mzima wa Sha'abaan ni Makruhu (hakupendezi) na ni kinyume na Sunnah za Mjumbe wa Allaah (S.a.w).

Ibn 'Abbaas (R.a) amesema: “Msiutangulie Ramadhaan kwa (kufunga) siku moja au mbili, ila kwa wale tu wenye mazoea ya kufunga kila mara, na kwa hali hiyo hao wanaweza kufunga (siku hizo)” Al-Bukhaariy

## JE KATIKA NISFU SHAABAN KUNA UKWELI WOWOTE NDANI YAKE?

Pamoja na ubora huo na daraja hiyo ya mwezi wa Sha'abaan, Mtume (S.a.w) hakuihusisha siku maalum katika mwezi wa Shaaban kufunga. Alikuwa akifunga kwa wingi iwezekanavyo lakini hakutueleza na wala hakuichagua siku ya tarehe 15 ya Shaaban kufunga kutokana na sifa zake alizozitaja hapo nyuma, ila tu ametaja Fadhila za

usiku huu kutokana na hadiyth hii ambayo hata hivyo haikutaja kuwa kuna ibada maalum inapaswa ifanyike siku hii au usiku wake.

Imetoka kwa Abu Muusaa Al-Ash'ariy (R.a) kwamba Mtume (S.a.w) kasema: “Allaah Mtukufu Hutokea Katika usiku wa 15 wa Shaaban, na Huwasamehe wote isipokuwa Washirikina na wale wenye uadui kwa wengine.” Ibn Maajah na imesemwa kuwa ni Hadiyth Hasan na Shaykh Al-Albaaniy.

Jambo la kushangaza ni kwamba wengi katika Waislam kwa uchache wa elimu na pia kwa kufuata mafundisho yasiyo sahihi ambayo amesingiziwa nayo Mtume (S.a.w) wameitenga siku hiyo ya Nisfu Sha'abaan kufunga na kusimama kisimamo cha usiku na kusoma nyiradi mbalimbali ambazo wamezitunga na pia kusherehekea kwa namna mbalimbali. Sehemu nyingi ulimwenguni hufanya sherehe na Swawm pamoja na kuswali sana usiku kwa kuiadhimisha siku hiyo ambayo huamini ni ya aina yake.

Kuna waliyoipa jina la Shab-E-Baraat au Laylatul Bara-at (usiku wa kuachiwa huru [na moto], au wa kusamehewa) kama huko bara Hindi, Pakistan na Bangladesh. Na kwengine hujulikana zaidi kwa Nisfu Sha'abaan n.k. ambapo katika siku hiyo wanaamini kuwa ni siku ya kusamehewa kwani Allaah Anawaachia huru waja wake walio motoni kutokana na mojawapo ya Hadiyth zisizo sahihi zilizohusishwa na mwezi huu wa Sha'abaan kama hii “Allaah Anawaachia huru waja wake walio

motoni kulingana na idadi ya nywele zilizo katika ngozi za mbuzi/kondoo wa Banu Kalb.”

Vilevile kuna imani potofu kabisa katika siku hii, ambapo kuna baadhi ya watu wanaamini kuwa kushuka kwa Malaika na Ruuh usiku huo kama ilivyo katika Suratul-Qadr Aayah ya 4, wao wameelewa maana yake ni kuwa Ruuh iliyokusudiwa katika sura hiyo ni roho za wale waliokufa! Na kwamba 'roho' hizo zashushwa na kurejea duniani na kukutana na wake wa wenye hizo roho na jamaa zao wengine. Na kwa sababu hiyo, wale wajane hupika vyakula bora vilivyokuwa vikipendwa na hao waume zao waliokufa kisha huviandaa na kusubiri ziara zao kutoka huko walipo. Baadhi ya watu pia huzuru makaburi katika siku hiyo na kuwaombea msamaha wale wote waliokufa mwezi wa Shaaban uliopita na huo walio nao.

Tunamuomba Allah atupe nguvu tuweze kushikamana na Sunnah za Mtume wetu Muhammad (S.a.w) katika maisha yetu. Ameen!!.